

HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO

Barua zote ziandikwe kwa
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.
Simu No. 027-2539603/2
Fax: No. 027 - 2539603



S.L.P84,
Longido,
Mkoa wa Arusha.

11.07.2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Longido Kata ya **ELANG'ATADAPASH, OLMOLOG** na **KAMWANGA** inakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezp wa kujaza nafasi za Watendaji wa Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata hizo tatu kama ifuatavyo:-

1. Msimamizi wa Kituo cha Kupigia kura - nafasi 34

Sifa za Mwombaji.

- Elimu isiyopungua Kidato cha nne au kuhitimu Mafunzo ya Kitaaluma kutoka Shule au Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na masharti ya jumla yaliyopo kwenye tangazo hili.

2. Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha kupigia kura - Nafasi 68

Sifa za Mwombaji.

- Elimu isiyopungua Kidato cha nne au kuhitimu Mafunzo ya Kitaaluma kutoka Shule au Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na masharti ya jumla yaliyopo kwenye tangazo hili.

3. Karani Mwongozaji wa Kituo cha kupigia Kura - Nafasi 34

Sifa za Mwombaji.

- Elimu isiyopungua Kidato cha nne au kuhitimu Mafunzo ya Kitaaluma kutoka Shule au Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na masharti ya jumla yaliyopo kwenye tangazo hili.

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- ❖ Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa Miaka 18 na kuendelea.
- ❖ Waombaji wasiwe Viongozi wa Chama chochote cha Siasa.
- ❖ Waombaji wawe waadilifu, watiifu na wenye akili timamu.
- ❖ Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- ❖ Maombi yote yaambatane na Vyeti vya Taaluma, Nakala za Vyeti vya Kidato cha Nne/Sita au kuhitimu Mafunzo kwa kuzingatia Sifa walizonazo kwa mujibu wa tangazo hili.
- ❖ Waombaji waambatanishe picha tatu "Pasport Size" za hivi karibuni.
- ❖ Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za Kazi kwa waajiri wao.
- ❖ Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za Kisheria.
- ❖ Mwisho wa kutuma maombi ya Kazi ni tarehe 20.07.2018 saa 10:00 Jioni.

Anuani ya kutuma Maombi hayo ni:
Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Longido,
S.L.p 84,
Longido.


Jumaa M. Mhina,
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

